

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA

MKOZA WA DAR ES SALAAM

Anwani ya Simu:

Simu: 2203156/58

Fax: +25522203213

Tovuti: www.dsm.go.tz

Barua Pepe: ras@dsm.go.tz



OFISI YA MKUU WA MKOZA

3 Barabara ya Rashidi

Kawawa,

S.L.P 5429,

12880 -DAR ES SALAAM.

Tanzania

TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**RC MAKONDA ATOA SHEHENYA YA MIFUKO 1,200 YA SARUJI KWA
ASKARI 12 BORA.**

Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam Mhe. Paul Makonda leo Juni 24/ 2018 ametimiza ametimiza ahadi yake kwa Jeshi la Polisi aliyoitoa hivi karibuni kwa kuwakabidhi shehena ya Mifuko 1,200 ya Saruji sawa na Tani 60 yenye thamani ya shilingi Milioni 14 kwa Askari Bora 12 waliochaguliwa na Jeshi la Polisi kutokana na utendaji kazi mzuri.

RC Makonda amesema lengo la kutoa zawihi hiyo ni kujenga morali ya kazi kwa askari wanaojitoa kwa hali na Mali kulinda usalama wa Raia na Mali zao jambo linalopelekea Dar es salaam kuwa Shwari.

Mifuko hiyo ya Saruji imetolewa na kampuni ya Nabis Cooperate Ltd iliyounga mkono jitiada za RC Makonda katika kugusa maisha ya Wananchi katika masuala mbalimbali.

Aidha RC Makonda amesema pamoja na kuendelea kuliboresha Jeshi la Polisi Kama taasisi kwa kuwapatia vitendea kazi Kama Magari, Pikipiki, Baiskeli na Computer pia ameona ni vyema kugusa maisha ya askari mmojammoja kwa kuhakikisha wanakuwa na makazi zao na familia ili familia ijivunie kazi anayoifanya Baba au Mama.

Hadi sasa RC Makonda amewezesha zaidi ya askari Polisi 800 kupata mikopo ya viwanja vya bei nafuu.

Kwa upande wake Mkurugenzi wa Kampuni ya Nabis Cooperate Ltd Eng. Thomas Wiso amesema kuwa wameamua kutoa saruji hiyo kuunga mkono jitiada za RC Makonda kujali wananchi wake na kuhakikisha hali ya Ulinzi na usalama inakuwa Shwari.

Imetolewa na:-

Kitengo cha Habari na Uhuisiano

OFISI YA MKUU WA MKOA

DAR ES SALAAM

24/06/2018